# *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Simu: +255 (0)22-2122722/3
Nukushi: +255 (0)22-2130852
Barua pepe: dg@nbs.go.tz
Tovuti: www.nbs.go.tz

18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796,
11992 - Dar es Salaam,
**TANZANIA.**

*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb. Na. NBS/N.20/2/

Tarehe: 26 Februari, 2015

## TAARIFA KWA UMMA

## PATO LA TAIFA ROBO YA TATU YA MWAKA (JULAI – SEPTEMBA) 2014


Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina jukumu la kukokotoa na kusambaza takwimu rasmi nchini ikiwa ni pamoja na takwimu za Pato la Taifa kwa robo Mwaka. Takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka hupimwa kwa kuangalia thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa nchini katika vipindi vya miezi mitatu mitatu ambavyo ni Januari – Machi, Aprili – Juni, Julai – Septemba na Oktoba - Desemba. Utayarishaji wa takwimu za Pato la Taifa hujumuisha shughuli zote za kiuchumi na hivyo hutumika katika kutathmini, kupanga mipango na kutayarisha sera za kiuchumi.

Takwimu za robo mwaka ya tatu zinazowasilishwa leo hii (Julai – Septemba) kwa ***bei za miaka inayohusika na mwaka wa 2007 zinasambazwa kwa mara ya kwanza*** ambazo zimetayarishwa kwa kuzingatia marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007.

Matokeo ya takwimu za Pato la Taifa kwa robo mwaka kwa bei za miaka inayohusika yameonyesha kuwa thamani ya Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ilikuwa TZS 21.0 trilioni mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS 19.4 trilioni kwa mwaka 2013.

Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007 katika kipindi cha robo mwaka ya tatu linaonyesha kuwa na jumla ya thamani ya TZS 10.7 trilioni kwa mwaka 2014 ikilinganishwa na TZS 10.0 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2013, hii inamaanisha kuwa Pato la Taifa liliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.8 katika kipindi cha robo ya tatu mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

**Kielelezo 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo ya Tatu, Julai – Septemba, 2006 – 2014**




## UKUAJI WA PATO LA TAIFA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

### *Ukuaji wa Sekta ya Kilimo na Mifugo*

Shughuli za kiuchumi za kilimo na mifugo zilikua kwa kasi ya asilimia 2.0 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 3.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Katika kipindi husika, kilimo cha **Mazao** kilikua kwa asilimia 2.4 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2013;  Ukuaji wa shughuli za **Ufugaji** uliongezeka kwa asilimia 2.1 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2013; ukuaji wa shughuli za **Misitu** uliongezeka kwa asilimia 0.3 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia hasi 0.9 mwaka 2013.

Shughuli za **Uvuvi** ziliongezeka kwa asilimia hasi 0.3 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2013.

Ukuaji sekta ya kilimo na mifugo ulitokana na jitihada za serikali kuwasaidia wakulima kwa kutoa ruzuku na maelekezo ya ma-ofisa Ugani kwa wakulima kama vile kuchagua mbegu bora yalisaidia kuongeza uzalishaji.

***Shughuli za Uchumi za Viwanda na Ujenzi***

Shughuli za **Uchimbaji Madini, Mawe** na **Kokoto** ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.2 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 3.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Uzalishaji wa dhahabu katika kipindi cha robo ya tatu kwa mwaka 2014 ulikuwa kg 10,137 ikilinganishwa na kg 11,010 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Uzalishaji wa Almasi katika kipindi cha robo ya tatu 2014 ulikuwa karati 66,508 ikilinganishwa na karati 27,828 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Madini ya Tanzanite yaliyozalishwa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 yalikuwa kg 1,449 ikilinganishwa na kg 5,140 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Shughuli za **Uzalishaji bidhaa Viwandani** zilikua kwa kasi ya asilimia 10.8 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.4 mwaka 2013. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za vyakula, tumbaku, nguo,na simenti.

Shughuli za **Uzalishaji nishati ya umeme** zilikua kwa kasi ya asilimia 10.7 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 10.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Kuongezeka kwa ukuaji wa nishati ya umeme kulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme unaotokana na mafuta na gesi.

Kwa upande mwingine, shughuli za **Usambazaji Maji** ziliongezeka kwa asilimia 12.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2013.

Shughuli za **Ujenzi** (ambazo zinajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi na zisizo za makazi; barabara na madaraja; na shughuli nyingine za uhandisi) katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 zilikua kwa asilimia 15.0 ikilinganishwa na asilimia 16.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

***Ukuaji wa Shughuli za Uchumi za Utoaji Huduma***

Shughuli za **Biashara za jumla na reja reja, Ukarabati wa Magari na Pikipiki na Vifaa vingine vya Nyumbani** zilikua kwa kasi ya asilimia 6.0 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Shughuli za **Uchukuzi na Uhifadhi** zilikua kwa kasi ya asilimia 16.0 katika kipindi cha robo ya

tatu ya mwaka 2014 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 19.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013.

Shughuli nyingine kama vile huduma za **Malazi na Chakula** zilikua kwa kasi ya 0.2 ikilinganishwa na asilimia hasi 0.4, shughuli za **Habari na Mawasiliano** zilikua kwa asilimia 11.9 katika robo mwaka ya tatu 2014 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2013.

Shughuli za **Fedha na Bima** katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2014 ziliongezeka kwa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 6.8. **Upangishaji nyumba** asilimia 2.2 ikilinganishwa na asilimia 2.1, **Huduma za kitaalaamu; Kisayansi na Ufundi; Utawala na huduma nyinginezo** zilikua kwa asilimia asilimia 5.4 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia hasi 1.0 mwaka 2013.

Aidha, Shughuli za **Uendeshaji Serikali** zilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2013. Huduma za **Elimu** zilikua kwa asilimia 3.7 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2013, huduma za **Afya** asilimia 8.1 ikilinganishwa na asilimia 8.5 na shughuli za **Sanaa na Michezo** zilikua kwa asilimia 2.5 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2013, **Huduma nyinginezo** zilikua kwa asilimia 6.7 mwaka 2014 ikilinganishwa na asilimia 6.6 mwaka 2013 na shughuli nyingine za **Kaya zinazoajiri** zilikua kwa kasi ya asilimia 2.7 mwaka 2014 katika kipindi husika sawa na ukuaji kama huo mwaka 2013.

**Kwa mawasiliano:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu,**
**Dar es Salaam.**